THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

FASIHI YA KISWAHILI
School Based Assessment
Gredi ya 10
2026
Kazimradi

Jina la Mtathminiwa: _____Nambari ya Tathmini: _____

Jina la Shule : _____ Tarehe : _____Sahihi :_____

Maelekezo ya Kazimradi

a. Hii ni kazimradi binafsi.
b. Kazimradi hii ina mazoezi manne.
c. Mazoezi yote kwenye kazimradi hii ni ya lazima.
d. Kwa kila zoezi, hifadhi ithibati ya kazi uliyotekeleza kwenye potifolio ya tathmini.
e. Umilisi wa kimsingi utatathminiwa katika zoezi la 3.
f. Baada ya kukamilika kwa kazimradi, unahitajika kuwa na potifolio iliyo na yafuatayo.
    i. Maandishi ya awali kuhusu matayarisho ya utafiti.
    ii. Mbinu ulizotumia kukusanya habari.
    iii. Wimbo uliouandika katika lugha asilia.
    iv. Tafsiri ya Kiswahili ya wimbo uliouandika.
    v. Nakala ya awali zaidi ya ripoti ya utafiti.
    vi. Nakala safi ya ripoti.

Kwa matumizi ya mtathimini pekee		
	Upeo	**Alama ya Mtathminiwa**
Zoezi la 1	**10**	
Zoezi la 2	**15**	
Zoezi la 3	**20**	
Zoezi la 4	**15**	
Jumla	**60**	

Tathmini hii ina kurasa 6 zilizopigwa chapa.

© 2026 The Kenya National Examinations Council

Maagizo kwa Mtathminiwa kuhusu tathmini hii.

1. Tathmini hii ina mazoezi manne.

Zoezi la 1: Kufanya utafiti kuhusu moja kati ya aina za nyimbo katika jamii (alama10)

Zoezi la 2: Kufanya uchanganuzi wa wimbo uliofanyiwa utafiti (alama 15)

Zoezi la 3: Kuwasilisha wimbo uliofanyiwa utafiti (alama 20)

Zoezo la 4: Kuandika ripoti ya utafiti uliofanywa (alama 15)

2. Tekeleza shughuli kulingana na maagizo ya kila zoezi.

Suala kuu: Utafiti kuhusu nafasi na uwasilishaji wa aina mahususi za nyimbo katika jamii

Madhumuni ya kazimradi

Utafiti huu utakuwezesha kutathmini na kuthamini nafasi ya nyimbo katika jamii kwa kukusanya habari kuhusu sifa na umuhimu wa nyimbo hizo. Aidha utaweza kutambua muktadha wa kijamii ambamo nyimbo hizo ziliimbwa, kuangazia na kuchanganua ujumbe na vipengele vya uwasilishaji wa nyimbo hizo.

1. **Zoezi la 1:** Kufanya utafiti kuhusu moja kati ya aina za nyimbo katika jamii

a) Teua moja kati ya aina za nyimbo zifuatazo katika jamii yako.

   i. bembelezi

   ii. nyimbo za watoto

   iii. nyimbo za kazi

   iv. nyimbo za dini

b) Fanya utafiti kuhusu wimbo ulioteua kwa kuzingatia yafuatayo:

   i. Aina ya wimbo

   ii. Waliouimba wimbo huo

   iii. Walioimbiwa wimbo huo

   iv. Sababu ya kuuimba wimbo huo

   v. Wakati wimbo huo ulipoimbwa

   vi. Mahali wimbo huo ulikoimbiwa

   vii. Utamaduni unaohusishwa na wimbo huo

   viii. Historia inayohusishwa na wimbo huo

Unaweza kuwahoji wazazi/walezi, walimu, wasanii na wanajamii wengine wenye uelewa wa mada hii. Unaweza pia kusakura mtandaoni, kutafiti maktabani au kushiriki uimbaji na wenzako au wanajamii.

d) Andika kwa lugha asilia kisha uutafsiri, wimbo ulioufanyia utafiti. Unaweza:

i. kuuhifadhi kwenye daftari lako la utafiti au shajara
ii. kupiga chapa katika kifaa cha kidijitali
iii. kujirekodi ukiimba na kuweka rekodi hiyo

e) Mkiwa kwenye vikundi, jadilini kuhusu hoja ambazo kila mmoja alipata katika utafiti wake kwenye Zoezi la 1.

f) Kwa kuzingatia maoni ya wenzako, andika upya kazi yako kuhusu zoezi la 1.

g) Hifadhi kazi yako kwenye faili ya tathmini (potifolio). Hakikisha pia umehifadhi maoni ya wanafunzi wenzako.

2. Zoezi 2: Uchanganuzi wa wimbo

a) Changanua vipengele vifuatavyo katika wimbo ambao uliufanyia utafiti:
   i. Ujumbe/maudhui katika wimbo huo
   ii. Sifa za nyimbo za aina hiyo
   iii. Umuhimu wa wimbo huo katika jamii
   iv. Mitindo ambayo jamii ilitumia kuwasilisha aina ya wimbo uliotafitia
b) Mkiwa kwenye vikundi, jadilini kuhusu hoja ambazo kila mmoja alipata katika uchanganuzi wake kwenye zoezi la 2.
c) Kwa kuzingatia maoni ya wenzako, andika upya hoja zako kuhusu zoezi la 2.
d) **Hifadhi kazi yako kwenye faili ya tathmini (potifolio). Hakikisha pia umehifadhi maoni ya wanafunzi wenzako**.

3. Zoezi la 3: Uwasilishaji wa wimbo

a) Washirikishe wenzako kuimba wimbo ulioutafitia. Wenzako pia watawawasilishia huku mkishiriki. Unaweza kuimba kwa lugha asilia au ukaimba tafsiri ya lugha ya Kiswahili uliyoiandika.
b) Waombe wenzako wachukue video wakati unapoimba. Sikiliza wimbo uliorekodiwa kisha uboreshe uwasilishaji pale panapohitajika.
c) Mkiwa katika vikundi, tathmini wasilisho la kila mmoja wenu mkizingatia:
   i. Kupandishwa na kushushwa kwa sauti
   ii. Matumizi ya ishara za mwili na uso
   iii. Matamizi ya sauti yenye mdundo wa kimuziki
   iv. Matamshi ya maneno
   v. Matumizi ya vipengele vya lugha vinavyoibua hisia zifaazo
   vi. Matumizi ya kasi ifaayo ya wimbo
   vii. Mtiririko ufaao
   viii. Kushirikishwa kwa hadhira
d) Fanya mazoezi ya kuboresha uwasilishaji wako.
e) Mwasilishie mwalimu wimbo (imba wimbo) ulioutafitia ukizingatia mbinu zifaazo za uwasilishaji.
f) Mwalimu atatathmini uwasilishaji wako.
g) Mbali na vipengele vingine vya uwasilishaji wa aina ya wimbo uliomwimbia, mwalimu atatathmini umilisi wa kimsingi ufuatao:
   i. Kujiamini
   ii. Mawasiliano na ushirikiano

iii. Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo
iv. Ubunifu

4. Zoezi la 4: Uandishi wa Ripoti

a) Andika ripoti ya utafiti uliofanya kuhusu wimbo ulioteua. Ripoti hiyo iwe na sehemu zifuatazo:

i. Mada ya utafiti
Sehemu hii ijumuishe:

- Aina ya wimbo ambao unatafiti kuhusu
- Jamii inayowakilishwa na wimbo huo

ii. Utangulizi
Uonyeshe:

- Ulitafiti kuhusu aina ipi ya wimbo?
- Ulitumia mbinu zipi?
- Walengwa/ ulihoji nani/ ulishiriki na kina nani katika uwasilishaji wa wimbo huo?
- Ulifanya utafiti wapi?

iii. Matokeo ya utafiti
Yahusu wimbo mahususi ulioutafitia. Kwa mfano:

Nyimbo za kazi katika jamii hiyo:

- Zina historia ipi?
- Zilikuwa na maudhui na ujumbe upi?
- Ziliimbwa na nani?
- Ziliimbiwa wapi?
- Ziliimbwa katika muktadha gani wa jamii hiyo?
- Zililenga kupitisha ujumbe au maudhui yapi?
- Zilikuwa na sifa zipi?
- Kwa nini hasa jamii ikaziimba?
- Ziliwasilishwa kwa mitindo ipi?

iv. Hitimisho
Ijumuishe:

- muhtasari wa kazi nzima
- maoni yako binafsi kuhusu umuhimu wa kazimradi
- mchango wa kazimradi katika kuendeleza ujifunzaji

v. Mapendekezo
Onyesha kwa mfano,

- kipengele cha aina hii ya wimbo ambacho hukutafitia ambao ungependa kutafitia baadaye
- aina nyingine za nyimbo ambazo hukutafitia na ambazo ungependa zitafitiwe
- mkabala mwingine wa kutafiti kuhusu aina ya wimbo uliotafitia. Kwa mfano, kulinganisha ujumbe wa aina hii ya wimbo katika jamii mbili tofauti.

b) Wawasilishie wenzako ripoti uliyoandika ili wakutolee maoni ya kuiboresha. Wenzako pia watawasilisha ripoti zao. Zingatieni vipengele kwenye jedwali lifuatalo:

Kipengele cha Ripoti	**Kipengele mahususi cha kuzingatia**
Anwani	Mada ya utafiti ibainike. Aina ya wimbo unaotafitiwa ibainike. Kwa mfano: **Utafiti wa ujumbe, sifa, dhima na uwasilishaji wa bembelezi katika jamii ya Wabukusu.**
Utangulizi	Yafuatayo yadhihirike: Ameonyesha: i. alitafiti kuhusu wimbo upi? ii. alitumia mbinu ipi? iii. alihoji nani (walengwa)? iv. alifanya utafiti wapi?
Mwili	Ameonyesha matokeo ya utafiti kama ifuatavyo: Aina ya wimbo aliotafitia: • Una historia ipi? • Ulikuwa na maudhui na ujumbe upi? • Uliimbwa na nani/walengwa • Uliimbiwa wapi? • Uliimbwa katika miktadha gani wa jamii hiyo? • Ulilenga kupitisha ujumbe, maudhui au maadili yapi? • Ulikuwa na sifa zipi? • Kwa nini hasa jamii ikauimba? • Uliwasilishwa kwa mitindo ipi?
Hitimisho	Amedhihirisha: i. muhtasari wa kazi nzima ii. maoni yake binafsi kuhusu umuhimu wa kazimradi hiyo iii. mchango wa kazimradi hiyo katika kuendeleza ujifunzaji
Mapendekezo	Ameonyesha kwa mfano: i. kipengele cha aina hii ya wimbo ambacho hakutafitia ambacho angependa kutafitia baadaye. ii. aina nyingine za nyimbo za jamii ambazo hakutafitia na kupendekeza utafiti wa baadaye.

c) Boresha ripoti yako kulingana na maoni ya wenzako.
d) Andika nakala safi ya ripoti yako ukijumuisha maoni ya wenzako na maoni ya mwalimu.
e) Unaweza kupiga chapa ripoti yako na kuihifadhi kwenye kifaa cha kidijitali au kiungo maalum kwenye mtandao. Unaweza pia kutoa nakala na kuhifadhi kwenye faili ya tathmini.

Ithibati ya Utendaji

Kwa kila zoezi, sharti uwe na ithibati kwamba ulitekeleza shughuli kulingana na maagizo uliyopewa. Ithibati hizo zihifadhiwe kwenye faili ya tathmini (potifolio). Faili iwe na:

a. maandishi ya awali kuhusu matayarisho ya utafiti. Kwa mfano:
    i. orodha ya aina za nyimbo katika jamii yako
    ii. wimbo ulioteua
b. mbinu za kukusanyia habari, kwa mfano maswali ya mahojiano, hojaji rekodi ya mahojiano, rekodi ya wimbo ukiimbwa
c. wimbo uliouandika katika lugha asilia
d. tafsiri ya Kiswahili ya wimbo uliouandika
e. nakala ya awali zaidi ya ripoti ya utafiti
f. ripoti uliyoiandaa baada ya kujumuisha maoni ya wenzako na maelekezo ya mwalimu baada ya wasilisho lako
g. nakala safi ya ripoti uliyoiandaa baada ya kujumuisha mapendekezo ya mwalimu baada ya wasilisho lako

Tanbihi

Unaweza kuwa na potifolio ya kidijitali.

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.